Nuru ya Kiswahili, Juzuu 3(2), Desemba 2024: 24-44
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru32.2444

# Tathmini ya Nafasi ya Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

**Idahemuka Magnifique**
**Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Rwanda**
magnifiqueidahemuka@gmail.com

**na**

**Wallace K. Mlaga**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Rwanda**
w.mlaga@ur.ac.rw

## Ikisiri

Makala hii inajadili nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza nchini Rwanda. Ili kutimiza lengo hili, Nadharia ya Mawasiliano ya Scudder (1980) imetumiwa. Aidha, katika ukusanyaji data, mbinu za usaili, ushuhudiaji na uchambuzi matini zilitumiwa. Wango la utafiti lilihusisha walimu wa Kiswahili na wanafunzi wanaojifunza kwenye mchepuo wa Fasihi katika Kiingereza, Kifaransa, Kiswahili na Kinyarwanda (LFK). Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa ili kupata sampuli ya walimu 9 na wanafunzi 93. Makala inabainisha kwamba fasihi andishi ina nafasi katika ukuzaji wa uwezo wa mawasiliano, stadi za lugha, ujasiri na utambuzi wa hisia. Pia, sehemu kubwa ya walimu wa Kiswahili haijafanikiwa kutumia fasihi andishi katika kukuza stadi za mawasiliano katika Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wao; badala yake hujikita zaidi katika kufundisha dhana za nadharia ya fasihi. Aidha, makala inabainisha kuwa walimu wa shule teule hawajumuishi kikamilifu fasihi andishi katika mbinu zao za ufundishaji, wakizingatia zaidi kanuni za fasihi na kupuuza mazoezi ya mawasiliano ya kina. Tathmini za walimu zinaangazia zaidi stadi za kusoma na kuandika, huku zikipuuzia stadi nyingine kama vile kusikiliza, kuzungumza, ujasiri na utambuzi wa hisia ambazo ni stadi muhimu katika mawasiliano.

**Dhana za Msingi**: Fasihi andishi, mawasiliano, stadi za mawasiliano

## Utangulizi

Mawasiliano ni mchakato wa kuhamisha habari kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia ya maneno au ishara (Nguyen, Warren & Fehring, 2014). Stadi za mawasiliano zinajumuisha uwezo wa kuelewa, kujibu, na kutoa taarifa kwa ufanisi kwa kutumia lugha, ishara, au njia nyingine za mawasiliano (Ngọc, 2021). Stadi hizi zinahusisha kusikiliza kwa makini, kuwasiliana kwa uwazi kutumia lugha yenye heshima na staha, na kuwasiliana kwa ufanisi na watu kutoka mazingira mbalimbali. Pia, stadi za mawasiliano zinajumuisha utambuzi wa hisia na ujasiri.

Katika karne ya 21, wataalamu mbalimbali wamependekeza stadi ambazo kila mhitimu anapaswa kuwa nazo ili kufanikiwa katika soko la ajira. Stadi hizo ni tafakuri bunifu, tafakuri tunduizi, utafiti, utatuzi wa matatizo, mawasiliano, ushirikiano, utambuzi wa kijamii, utawala binafsi, TEHAMA na ujifunzaji wa muda mrefu (Erdem, Bağcı, Koçyiğit, Altıner, Saykili, Polat & Eğmir, 2019). Japokuwa stadi hizi ni nyingi, stadi za mawasiliano ni muhimu zaidi, kwani zinashiriki katika ukuzaji wa stadi nyingine kama utatuzi wa matatizo, ubunifu na ushirikiano (Derakhshan, Tahery & Mirarab, 2015). Gomatam (2015) anasisitiza kuwa stadi za mawasiliano ni muhimu sana katika maisha ya kibinafsi na kitaaluma, kwani husaidia kujenga mahusiano mema na kufanikisha utimizaji wa majukumu mbalimbali ya kimaisha.

Kwa mujibu wa Sarpparaje (2019), stadi za mawasiliano ni muhimu kwa wahitimu wote wa shule za sekondari zikiwamo za michepuo ya lugha. Aidha, stadi za mawasiliano zinahitajika katika maeneo mbalimbali kama sheria, elimu, serikali na teknolojia (Erdem na wenzake, 2019). Vilevile,

Pradesh, Toppo, & Philomina (2021) wanaonesha kuwa wahitimu wengi wa elimu katika shule za sekondari hawana stadi za mawasiliano. Hii inaathiri sana mafanikio yao kwa kuwapunguzia uwezo wa kujiamini (Sridhar, 2012). Hii ni kwa sababu, baadhi ya mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji wa lugha zinajikita katika maarifa ya kitaaluma na nadharia badala ya mafunzo ya vitendo ya ukuzaji wa stadi za mawasiliano (Rachella, 2021).

Aidha, Khakasa (2018) anaeleza kuwa kuna changamoto katika ufundishaji wa stadi za mawasiliano katika Kiswahili, ambapo mkazo mkubwa unawekwa kwenye kusoma na kuandika kuliko stadi nyingine muhimu kama vile kusikiliza kwa makini, kuzungumza kwa ufasaha, kufahamu hisia, ujasiri na matumizi ya ishara katika mawasiliano.

Kwa hiyo, ufundishaji wa fasihi simulizi na andishi unaweza kutumiwa katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari (Figueroa-Macias & Andrade-Zambrano, 2022 na Bisamaza, 2022). Licha ya maelezo ya watalaamu hawa, bado kuna mapengo kwa kuwa zinazungumzia fasihi kwa ujumla bila kuhusisha fasihi mahususi. Tena, zinajikita katika lugha ya Kiingereza ambayo ni tofauti na lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, tuliamua kufanya utafiti wetu kwa ajili ya kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza.

**Methodolojia na Nadharia ya Utafiti**

Ili kukamilisha lengo la utafiti, Nadharia ya Mawasiliano ya S. F. Scudder (1980) ilitumiwa. Nadharia hii inasisitiza kuwa mawasiliano ni muhimu katika maisha, yakielezewa kama mchakato wa kuhamisha mawazo na hisia kutoka kwa mtumaji hadi mpokeaji. Aidha, mawasiliano yanakuwa yenye mafanikio iwapo mpokeaji anaweza kufafanua ujumbe aliopewa. Mihimili

hii ya nadharia ilisaidia kutathmini jinsi fasihi andishi inavyoweza kuchangia katika kukuza stadi za mawasiliano katika shule za sekondari wilayani Nyanza, Rwanda.

Data za utafiti ulioibua makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini, usaili na ushuhudiaji. Uchanganuzi matini ulijikita kwenye matini za kitaaluma na kwenye matini za kipedagojia za walimu wa fasihi. Sampuli ya utafiti ilihusisha walimu wa Kiswahili 9 na wanafunzi 93 kutoka shule za CXR Nyanza, E.S. Nyanza, na G.S. Kigoma. Shule hizi zilichaguliwa kwa makusudi kwa kuwa ndizo shule zenye wanafunzi wanaojifunza katika mchepuo wa LFK, ambapo fasihi andishi ya Kiswahili hufundishwa. Wanafunzi wote wa kidato cha tano waliteuliwa kwa sababu ndio wanaojifunza fasihi andishi kwa kina, ikilinganishwa na wanafunzi wa kidato cha nne na cha sita katika mchepuo wa LFK. Sampuli ya wanafunzi ilihusisha wanafunzi 30 kutoka CXR Nyanza, 25 kutoka E.S. Nyanza, na 38 kutoka G.S. Kigoma.

## Tathmini ya Nafasi ya Fasihi Andishi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

Stadi za mawasiliano zinahusisha uwezo wa kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali, ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha ya mwili, toni ya sauti, na uwasilishaji wa ujumbe kwa uwazi na kueleweka (Seiler & Beall, 2011). Ngọc (2021) anaongeza kuwa stadi hizi zinajumuisha uwezo wa kuelewa, kujibu, na kutoa taarifa kwa ufanisi kwa kutumia lugha, ishara, na njia nyingine za mawasiliano. Makala hii inalenga kutathmini nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili kwenye shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Mjadala wa makala hii unaongozwa na mhimili wa kwanza wa Nadharia ya

Mawasiliano iliyoasisiwa na Scudder (1980). Mhimili huu unasema kwamba mawasiliano ni mchakato wa kiufundi wa kuhamisha mawazo, ujumbe na hisia kutoka kwa mtu mmoja mmoja kwenda kwa mwingine. Hoja zinazowasilishwa ni pamoja na fasihi andishi katika kukuza uwezo wa vipengele vifuatavyo: mawasiliano, stadi za lugha, stadi ya ujasiri, na stadi ya utambuzi wa hisia.

**Fasihi andishi katika kukuza uwezo wa mawasiliano**

Taarifa zilizopatikana kutoka katika uchanganuzi wa matini za kitaaluma zimehusisha watafiti tangulizi ambao walijaribu kushughulikia nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za lugha. Aidha, baadhi ya watafiti, kama vile Priyadharshini, & Hameed (2018), wamebainisha kwamba fasihi andishi ina nafasi ya kukuza uwezo wa kusikiliza na kuandika ambao unahitajika katika mawasiliano. Hata hivyo, hali halisi kwenye shule za sekondari teule wilani Nyanza inaonesha kwamba bado fasihi andishi haina nafasi inayostahili katika ukuzaji wa uwezo wa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Wakionesha hali hii, Priyadharshini, & Hameed (2018) wanasisitiza kuwa viongozi waliobarikiwa na kipawa cha kuongea huuingia mioyoni mwa watu kupitia stadi zao za mawasiliano. Sababu moja kuu inahusishwa kwa uaminifu na kusoma fasihi. Uwezo wa kuwasiliana ni mojawapo ya sifa zinazotamaniwa za uongozi. Wanaongeza kuwa kusoma humfanya mtu kuwa kamili; kuandika humfanya mtu kuwa sahihi. Ili kuwa mwasilianaji mzuri, mtu lazima awe kamili na sahihi pia. Kusoma na kuandika, ujuzi wa lugha wa uzalishaji katika mawasiliano unaweza kuendelezwa vyema kupitia kusoma fasihi.

Sharma, Dangoria & Jain (2022) wanaongeza kwamba fasihi andishi huwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa mawasiliano kwa kuimarisha

umahiri wao wa kipragmatiki. Huwapa wanafunzi uwezo wa kuelewa na kuwasilisha maana ambazo ni sahihi zaidi na zinazokubalika katika muktadha wa kitamaduni na kijamii. Hivyo, fasihi inaboresha uwezo wa wanafunzi katika mawasiliano kwa kuimarisha umahiri wao wa kipragmatiki. Hii ina maana kwamba fasihi inawasaidia kuelewa na kuwasiliana kwa ufanisi katika muktadha wa kitamaduni na kijamii. Fikra hizi zinathibitishwa pia na M1 (ambaye ni mtoataarifa mmojawapo). Anasema:

> Nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano ni kuwapa wanafunzi uwezo wa kuwasiliana kwa ufasaha. Kupitia ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, wanafunzi wanajifunza kanuni zote za mawasiliano, hali inayowafanya kuwa wataalamu wa mawasiliano (Data za uwandani, 2024).

Kutokana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tunaona kwamba kwamba fasihi andishi ina nafasi muhimu katika kuboresha stadi za mawasiliano kwa kuwapa wanafunzi ujuzi wa kuwasiliana kwa ufasaha. Kupitia mafunzo ya fasihi, wanafunzi wanajifunza kanuni za mawasiliano ambazo zinawawezesha kuwa wataalamu bora katika eneo hili.

Matini za kitaaluma na maoni ya walimu huonesha kuwa fasihi andishi ina nafasi muhimu katika kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi, lakini utafiti uliozalisha makala hii ulibaini kuwa walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza hawajumuishi kikamilifu ukuzaji wa stadi hizo katika ufundishaji wao. Badala ya kutumia tanzu za fasihi kukuza mawasiliano, walimu wanajikita zaidi kwenye ufundishaji wa kanuni za fasihi, na hivyo wanafunzi wanakosa mazoezi muhimu ya kuwasiliana kwa ufasaha.

Maelezo haya yanaungwa mkono na uchambuzi wa ushuhudiaji uliofanyika, ambapo asilimia 65 ya vipindi vilivyochunguzwa havikuhusisha mazoezi ya mawasiliano ya moja kwa moja. Matokeo haya yanaonesha hitaji la kubadilisha mbinu za ufundishaji ili fasihi andishi ichangie kikamilifu katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano.

Changamoto kubwa iliyobainika ni kwamba walimu wa Kiswahili wanahitaji mafunzo zaidi juu ya mbinu bora za kutumia fasihi andishi katika kukuza stadi za mawasiliano. Walimu walioshiriki kwenye utafiti walionesha kuwa kutojua mbinu bora ni kikwazo kikubwa. Pradesh, Toppon & Philomina (2021) wanasema kwamba ufundishaji wa stadi za mawasiliano unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ujuzi na maarifa katika matumizi ya mbinu mbalimbali na za kisasa za ufundishaji kama vile mawasilisho na mijadala, mafunzo ya kazi vitendo na matumizi programu za lugha na majukwaa ya mtandaoni. Mbinu hizi ni muhimu kwa kukuza ujasiri, kujieleza na mawasiliano ya kisasa ingawaje hazijatumika kikamilifu darasani. Hivyo, mabadiliko katika mbinu za ufundishaji yanahitajika ili kuhakikisha wanafunzi wanapata fursa za kukuza uwezo wa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Aidha, walimu kutoka kwenye shule za sekondari teule wanalazimika kutumia mbinu zinazokuza stadi za mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno kwa kuwapa wanafunzi fursa ya kuwasilisha kazi na kubadilishana mawazo katika Kiswahili. Hii, kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Mawasiliano, itawasaidia wanafunzi kumudu sheria za mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno.

**Fasihi andishi katika kukuza stadi za lugha**

Stadi za lugha zinahusu uwezo wa mtu kutumia lugha kwa usahihi na ufanisi, ambapo zinajumuisha kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na

kuandika (Sen, Mahendra, & Patnaik, 2015). Stadi hizi ni muhimu katika mawasiliano (Priyadharshini, & Hameed, 2018). Fasihi andishi ina nafasi muhimu katika kukuza stadi hizi za lugha. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba, kwenye shule za sekondari teule wialayani Nyanza, walimu wa Kiswahili wanatilia mkazo sana stadi za kusoma na kuandika wakisahau stadi nyingine faafu katika mawasiliano fasaha kwa lugha ya Kiswahili.

Priyadharshini & Hameed (whj) wanabainisha nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za lugha kwa kusema kuwa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika si stadi za mawasiliano, bali ni stadi za kujifunza lugha. Uwezo wa kuwasiliana hupatikana kupitia umahiri wa stadi za kujifunza lugha. Stadi hizi nne zote zina uhusiano wa karibu. Ingawa kuna mbinu nyingi za kufundisha na kujifunza lugha, mbinu inayotumia fasihi ina faida zake za kipekee ikilinganishwa na mbinu nyingine. Katika mbinu nyingine, lengo ni kukuza stadi na stadi ndogo za lugha lengwa, lakini katika mbinu inayotumia fasihi, wanafunzi, mbali na kukuza stadi za mawasiliano katika lugha lengwa, pia wanaelewa maisha na maadili ya kibinadamu. Licha ya hayo, stadi hizi zinashiriki katika mawasiliano fasaha katika lugha yoyote ile. Tunaona kwamba, mbinu inayotumia fasihi inatoa faida za kipekee kwa kukuza stadi hizi pamoja na ufahamu wa lugha, maisha na maadili ya kibinadamu.

Zaidi ya hayo, kwa kubainisha nafasi ya fasihi katika ujifunzaji wa lugha, Venkateswar & Mohana (2015) wanasema kwamba, kama mtu anataka kuwasiliana kwa ufasaha, ni lazima ajifunze fasihi. Kwa mujibu wa maoni yao, hali hii inasababisha na ukweli kuwa fasihi inahusisha herufi, maneno, virai, sentensi, aya, insha na hadithi. Katika kujifunza lugha, tunapaswa kuzingatia maeneo yote haya ya maarifa. Mawasiliano yanahusisha

mawazo, maoni, hisia na taarifa za kuchangia na wengine kwa madhumuni ya kibinafsi na kitaalamu. Vivyo hivyo na fasihi; ikiwa lugha ni akili, fasihi ni moyo. Lugha ni mfumo wa maneno, sarufi na muundo wa sentensi. Wanasisitiza kuwa yeyote anayetaka kuimarisha stadi za lugha kwa ajili ya mawasiliano, anapaswa kuzingatia hasa fasihi. Hapa tunaona kuwa fasihi ni muhimu katika kujifunza lugha kwani inajumuisha vipengele vyote vya lugha. Pia, tunaona kuwa yeyote anayetaka kuimarisha stadi za lugha hana budi kuzingatia fasihi kwa kuwa lugha ni mfumo wa maneno na sarufi, wakati fasihi ni moyo wa lugha hiyo. Hii inasisitiza nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za lugha zinazohitajika katika mawasiliano.

Zaidi ya hayo, data za usaili kutoka kwa walimu wa Kiswahili zinaonesha kuwa fasihi andishi huchangia kuwafundisha wanafunzi matumizi fasaha ya lugha, ikiwamo kusikiliza, kusoma, kuandika, na kuzungumza, huku wakizingatia muktadha wa kiutamaduni na kijamii. Mtoataarifa M3 anayakinisha kwa kusema:

> Fasihi andishi ina nafasi kubwa katika kufundisha wanafunzi jinsi ya kutumia lugha kwa ufanisi, iwe ni kwa maandishi au mazungumzo. Kupitia fasihi andishi, wanafunzi huimarisha vipengele muhimu vya mawasiliano, kama vile uwezo wa kuandika kwa mpangilio, ambapo wanajifunza kuwasilisha mawazo kwa uwazi na mantiki. Pia, huongeza ufahamu wa kusoma na kuchanganua maandishi kwa kina, wakitambua maana zilizojificha. Vilevile, fasihi andishi huwasaidia wanafunzi kutumia lugha inayoendana na muktadha wa kiutamaduni na kijamii, pamoja na kuimarisha uwasilishaji wa hoja kwa ufasaha, kwa njia ya maandishi au mazungumzo. Kwa njia hii, wanafunzi hujengewa uwezo wa kuwasiliana kwa ufanisi katika mazingira mbalimbali (Data za Uwandani, 2024).

Tunaona kwamba fasihi andishi ina nafasi kubwa katika kufundisha wanafunzi kutumia lugha kwa ufasaha, kusoma, na kuandika. Pia, inawasaidia kuwasiliana kwa kuzingatia muktadha wa kiutamaduni na kijamii. Ingawaje imebainika kwamba fasihi ina nafasi katika ukuzaji wa stadi za lugha zinazohitajika katika mawasiliano, uasili na walimu husika yalionesha mchanganyiko wa stadi za lugha na stadi za mawasiliano. Hii inatokana na mtazamo finyu wa stadi za lugha, unaozingatia sana kusoma, kuandika, kuzungumza na kusikiliza, ambazo ni sehemu tu za ujuzi wa lugha. Akitoa maoni kuhusu fikra hii, M1 (mtoatarifa ambaye ni Mwalimu) anasema:

> Stadi za mawasiliano ni stadi za kusikiliza, stadi za kuzungumza, stadi za kuandika na stadi za kusoma. Stadi za kusikiliza zinahusisha uwezo wa kuelewa na kufasiri ujumbe unaowasilishwa kwa njia ya maneno. Stadi za kuzungumza zinahusisha uwezo wa kueleza mawazo na hisia kwa njia ya maneno kwa ufasaha, stadi za kusoma zinahusisha uwezo wa kuelewa na kufasiri maandishi, na stadi za kuandika zinahusisha uwezo wa kuandika ujumbe kwa njia inayoweza kueleweka kwa wasomaji (Data za Uwandani, 2024).

Dondoo hili linatuonesha kwamba, stadi za mawasiliano zinahusisha stadi nne. Stadi ya kwanza ni stadi ya kuzungumza inayohusisha uwezo wa kusikiliza. Stadi ya pili ni stadi ya kusikiliza inayohusisha uwezo wa kuelewa na kufahamu ujumbe unaotolewa na mzungumzaji. Stadi ya tatu inahusisha stadi ya kusoma ambayo inahusisha uwezo wa kusoma maandishi. Stadi ya mwisho ni ya kuandika ambayo inahusisha uwezo wa kuawasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi. Ilibainika kwamba walimu wanapofundisha fasihi andishi, wanasisitiza tu ukuzaji wa stadi za lugha na

kusahau stadi nyingine muhimu katika mawasiliano kama vile stadi ya kusikiliza kwa makini, utambuzi wa hisia, na ujasiri.

Zaidi ya hayo, tathmini zinazoandaliwa na walimu wa fasihi zinahusisha sana ukuzaji wa stadi za kusoma, kufahamu maandishi na kuandika. Miongoni mwa tathmini za walimu 9 zilizochunguzwa, hakuna tathmini iliyohusisha kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza kwa makini, kuzungumza kwa ufasaha, ujasiri na stadi nyingine za mawasiliano yasiyo ya maneno. Hapo chini ni mojawapo ya tathmini zilizofanyiwa uchunguzi. Tathmini hiyo iliandaliwa na M8.

**Kielelezo Na. 1: Mfano wa Tathmini**

**SEHEMU YA IV: FASIHI** **(Alama 11)**

1) Je fasihi ni nini? **(Alama 1)**

2) Eleza tofauti iliyopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. **(Alalama 4)**

3) Fasihi ni kioo cha jamii. Jadili. **(Alama 4)**

4) Tofautisha tabia tatu za wahusika katika riwaya. **(Alama 3)**

**Chanzo:** Data za Uwandani (2024)

Kielelezo hiki kinaonesha tathmini ya fasihi inayojikita kwenye kupima stadi za kuandika na kusoma, huku ikipuuza stadi muhimu za kuzungumza, kusikiliza kwa makini, na ujasiri, ambazo ni muhimu kwa mawasiliano fasaha kwa lugha ya Kiswahili. Maswali yote yaliyoulizwa yanahitaji majibu ya maandishi na yanapima uwezo wa mwanafunzi katika kusoma na kuandika, bila kujumuisha mazoezi ya mawasiliano ya mdomo au uigizaji.

Kwa mujibu wa Khakasa (2018), kuna changamoto katika ufundishaji wa Kiswahili ambapo mkazo mkubwa unawekwa kwenye kusoma na kuandika kuliko stadi nyingine muhimu kama vile kusikiliza kwa makini, kuzungumza kwa ufasaha, kufahamu hisia, ujasiri, na matumizi ya ishara katika mawasiliano. Hivyo basi, ingawaje walimu wa Kiswahili wanafanya vizuri katika ufundishaji wa stadi za lugha zinazohitajika katika mawasiliano, kuna haja ya walimu hawa kubadilisha mbinu wanazotumia ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata mafunzo yanayowezesha kukuza stadi zote za mawasiliano kwa usawa na ufanisi.

**Fasihi andishi katika kukuza stadi ya ujasiri**

Ujasiri, kama stadi muhimu katika mawasiliano, inahusisha uwezo wa kuzungumza bila woga, kujieleza kwa uhakika, na kushiriki kikamilifu katika mazungumzo (Atkin, 2012). Utafiti uliozalisha makala hii umeonesha kwamba fasihi andishi ina nafasi muhimu katika kukuza stadi hii miongoni mwa wanafunzi. Hata hivyo, hali halisi kwenye shule za sekondari teule wilayani Nyanza inaonesha kwamba fasihi andishi ya Kiswahili haijawa na nafasi katika ukuzaji wa stadi ya ujasiri miongoni mwa wanafunzi wa shule hizi. Ilankumaran & Deepa (2018) wanabainisha nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi ya ujasiri kwenye dondoo lifuatalo:

> Fasihi ni muhimu katika darasa la lugha. Haiburudishi tu wasomaji bali pia huongeza ujasiri na kukuza uwezo wa kufikiri kwa kina. Zaidi ya hayo, fasihi inajumuisha aina mbalimbali kama vile nathari, mashairi, tamthilia, riwaya, hadithi fupi na nyinginezo. Aina hizi zinasaidia wanafunzi kuboresha stadi zao za mawasiliano na kupata uwezo wa kuwasiliana kwa ujasiri (uk. 620).

Tunaona kwamba fasihi andishi ni muhimu katika darasa la lugha kwani inasaidia kuongeza ujasiri na kukuza uwezo wa kufikiri na kuwasiliana kwa ujasiri.

Aidha, ufundishaji wa fasihi andishi unawalazimisha wanafunzi kusoma kazi za fasihi za aina mbalimbali. Usomaji hukuza stadi ya ujasiri. Hii ni kwa sababu humwezesha msomaji kugundua dunia mpya au kupata ujuzi mpya kupitia kusoma, lakini faida zake zinaenda mbali zaidi ya burudani na elimu ya kimsingi. Kusoma kunaathiri tabia kwa kina kwa kuboresha ujasiri, kupanua mtazamo wetu na kukuza uwezo binafsi. Maoni haya yalitiliwa nguvu na watoataarifa. Mathalani, M1 anasema:

> Ninadhani kuwa fasihi andishi inasaidia sana katika kuwezesha wanafunzi kuwasilisha mawazo yao bila wasiwasi. Kupitia kazi za fasihi, wanafunzi hujifunza jinsi ya kueleza hisia zao na maoni yao kwa ufasaha. Hivyo, mimi ninaona kwamba fasihi andishi ina nafasi muhimu katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wangu (Data za uwandani, 2024).

Data hii inatuonesha kwamba fasihi andishi inawasaidia wanafunzi kuwasilisha mawazo yao bila wasiwasi. Pia, huwasaidia wanafunzi kujifunza jinsi ya kueleza hisia na maoni yao. Mtoataarifa mwingine, M5, anaongezea:

> Nafasi ya fasihi andishi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano ni kukuza ujasiri wa wanafunzi. Mbinu za kusimulia hadithi fupi na uigizaji wa tamthilia zinajenga ujasiri wa wanafunzi katika kujieleza mbele ya wengine. Wanapopata uzoefu wa kujifunza na kushiriki katika tamthilia au hadithi, wanafunzi wanajenga ujasiri na uwezo wa kujieleza kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili (Data za uwandani, 2024).

Data hii inatuonesha kwamba mbinu za kusimulia hadithi fupi na uigizaji wa tamthilia zina nafasi kubwa katika kujenga ujasiri wa wanafunzi katika kujieleza kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, hali halisi kwenye shule za sekondari teule wilayani Nyanza inaonesha kwamba fasihi andishi haijatumika ipasavyo katika kukuza stadi ya ujasiri. Walimu wa fasihi wanakosa kuzingatia mbinu za kukuza stadi za mawasiliano; badala yake, wanajikita zaidi kwenye ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi pekee, hivyo kupuuza umuhimu wa maendeleo ya ujasiri wa wanafunzi.

Zaidi ya hayo, walimu hawahusishi ukuzaji wa stadi za mawasiliano, ikiwamo ujasiri katika maandalizi ya masomo. Hata na wale wanaojaribu kuhusisha stadi za mawasiliano hawaelewi maana ya mawasiliano. Miongoni mwa walimu walioshuhudiwa, hakuna yeyote ambaye alihusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano, ikiwamo ujasiri katika sehemu ya *Malengo ya Ujifunzaji*.

Utafiti ulibaini kuwa walimu hujaribu kuhusisha ukuzaji wa stadi husika kwenye sehemu ya *Uwezo wa Jumla na Maswala Mtambuka*. Hata hivyo, maelezo yanayotolewa yalibainika kutoendana na stadi za mawasiliano. Mfano mmojawapo ni wa andalio la somo lifuatalo la mtoataarifa M3 ambaye ni mwalimu:

**Kielelezo Na. 1: Mfano wa Andalio la Somo**

| Jina la Mwalimu: | | | | Shule: | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Muhula: | Tarehe: | Somo: | Kidato: | Mada: | Somo la: | Muda: | Idadi ya Wanafunzi |
| wa tatu | 6/6/2024 | KISWAHILI | 6 LFK | I... | I katika .5. | Dakika .40 | 23/25 |

| | |
|---|---|
| Aina ya wanafunzi wenye mahitaji ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao | Mwanafunzi mmoja mwenye ulemavu wa viungo vya mwili |
| Mada | Fasihi katika Kiswahili |
| Uwezo Upatikanaoo Katika somo | Mwanafunzi awe ze kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kutumia kanda mojawapo ya njia za kujitegemea maishani |
| Somo Lenyewe | Tanzu za Fasihi Andishi |
| Malengo ya Kujifunza | Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi awe ze: i) Kutofautisha kwa usahihi tanzu ya fasihi andishi ii) Kutambua kwa urahisi maana ya msamiati unaohusiana na tanzu za fasihi andishi |
| Mahali ambapo somo litafundishiwa | Darasani |
| Vifaa au zana kwa wanafunzi wote | Vitabu vya Kiswahili, nyaraka mbalimbali za fasihi, kamusi na mtandao |
| Vitabu vya rejelea | Kitabu cha Kiswahili 6, Kiswahili kwa shule za Rwanda 6, Kitabu cha malimu, Kigali & Kamusi ya Kiswahili TUKI (2019). |

| Muda na hatua | Mbinu za Kufundisia na Kujifunzia | | Uwezo wa Jumla na Maswala Mtambuka + Maelezo Mafupi |
|---|---|---|---|
| | Kwa kutumia vifungu vya habari tofauti, malimu atawawezesha wanafunzi kutofautisha kwa usahihi tanzu za fasihi andishi, kutambua kwa urahisi maana ya msamiati unaohusiana na tanzu za fasihi andishi. | | |
| | Majukumu ya Mwalimu | Majukumu ya Mwanafunzi | |
| Utangulizi Dakika .5... | Kusalimu na kuuliza maswali tangulizi yo kuingiza wanafunzi kwenye somo | Kusalimu mwalimu na kujibu maswali | Stadi za utafiti (kupitia kusoma na kujibu maswali, wanafunzi watakuza uwezo wa utafiti) |
| Somo lenyewe Dakika .25. | Kuwaingiza wanafunzi kwenye soma kifungu na kujibu maswali yanayoendana na kifungu. Kufuata kuwa kazi inafanyika makundini. Kutoa msaada panapohitajika na kuomba wanafunzi kuwasilisha kazi walizozi fanya. Kufupisha somo. | Kujibu maswali na kufuata. Kukaa kwa makundi ya wanafunzi watano, kusoma kifungu na kujibu maswali yanayoendana na kifungu. Kufanya kazi kuomba msaada panapohitajika na kuwasilisha kazi zao. Kushirikiana na mwalimu katika ufupishaji wa somo | Mawasiliano (kwa kufanya kazi za makundi, wanafunzi watakuza stadi za mawasiliano kwa kuchangia majukumu.) Elimu ya amani na maadili (kupitia usomaji wa kifungu cha habari, wanafunzi watakuza elimu ya amani na watakuza maadili yao.) |
| Hitimisho Dakika .10.. | Kutathmini kwa malengo ya kujifunza yametimizwa | Kufanya tathmini. | |
| Tathmini ya mwalimu | Somo limefundishwa vizuri | | |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2024)

Kutokana na andalio hili, tunaona kwamba mwalimu hakuhusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwenye malengo ya ujifunzaji. Ingawa mwalimu amehusisha ukuzaji wa stadi za mawasiliano kwenye andalio la somo lake (kwenye sehemu ya Uwezo wa Jumla na Maswala Mtambuka), maelezo aliyoyatoa hayahusiani na stadi za mawasiliano. Mwalimu huyu aliandika, “Mawasiliano (kwa kufanya kazi za makundi, wanafunzi watakuza stadi za

mawasiliano kwa kuchangia majukumu).” Mwalimu anayejihusisha na ufundishaji wa fasihi andishi anaonekana kuwa na uelewa hafifu kuhusu stadi za mawasiliano, kwani maelezo aliyoyatoa yanahusiana zaidi na stadi ya ushirikiano badala ya kukuza mawasiliano. Hii inaathiri ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Hata hivyo, licha ya kuwa Ilankumaran & Deepa (whj) wanasema kuwa uwasilishaji wa mashairi unaweza kukuza ujasiri, hii haijaonekana kutekelezwa katika shule za sekondari wilayani Nyanza kutokana na changamoto ya muda. Ushuhudiaji na usaili wa walimu unaonesha kuwa wanafunzi wanakosa fursa ya kushiriki katika uwasilishaji wa kazi za fasihi, hivyo kukosa nafasi ya kukuza stadi zao za ujasiri. Kwa hiyo, walimu wanalazimika kutumia muda wa ziada ili kila mwanafunzi apate nafasi ya kujieleza mbele ya wengine kwa ajili ya kukuza stadi ya ujasiri.

Hivyo basi, licha ya nafasi ya fasihi andishi ya kukuza stadi ya ujasiri, imebainika kwamba katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza bado fasihi haijakuwa na nafasi hii. Hii inatokana na walimu kutohusisha stadi za mawasiliano, ikiwamo ujasiri katika maandalio ya masomo ya fasihi andishi katika Kiswahili. Vilevile, wanakabiliwa na ufupi wa muda uliotengwa wa kufundisha somo la fasihi andishi. Mhimili wa pili wa Nadharia ya Mawasiliano unasisitiza kwamba mawasiliano ni mchakato wa kusambaza habari kutoka kwa mtumaji hadi mpokeaji ambaye anafafanua na kuchukua hatua kulingana na ujumbe alioupokea. Hali iliyobainika katika wilaya ya Nyanza inakinzana na mhimili huu. Walimu wanashindwa kuhakikisha kuwa mawasiliano kupitia fasihi andishi ni mchakato wa ufanisi unaowezesha wanafunzi kufafanua na kuchukua hatua kwa ujasiri kulingana na ujumbe wanaoupokea.

**Fasihi andishi katika kukuza stadi ya utambuzi wa hisia**

Johnson (2018) anaeleza kuwa utambuzi wa hisia ni uwezo wa kuelewa na kutambua hali za kihisia za watu wengine, hata bila ya maelezo ya wazi. Stadi hii ni muhimu katika mawasiliano, kwani inasaidia mtu kujibu hisia za wengine kwa ufasaha na kuboresha mawasiliano. Sehemu hii inatathmini jinsi fasihi andishi inavyosaidia kukuza stadi ya utambuzi wa hisia. Baadhi ya matini za kitaaluma zilizochanganuliwa zimeonesha kwamba fasihi andishi inaweza kukuza utambuzi wa hisia kwa wanafunzi. Johnson (*ameshatajwa*) anasisitiza jambo hili kwa kusema kuwa matini za fasihi hutoa nafasi kwa wanafunzi kuelewa na kujifunza kuhusu hisia za wahusika kupitia uandishi wa kina na usimulizi. Kwa kusoma na kuchanganua kazi za fasihi, wanafunzi wanapata uwezo wa kutambua na kuhisi hali za kihisia za wahusika, hivyo kuboresha utambuzi wao wa hisia. Hii inawasaidia kuboresha utambuzi wao wa hisia kwa kutambua na kuhisi hali za kihisia za wahusika. Akisisitiza kuhusu nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi ya utambuzi wa hisia, anasema:

> Fasihi inakuza stadi ya utambuzi wa hisia miongoni mwa wanafunzi. Fasihi inawasilisha hisia na hali za kihisia kupitia mbinu mbalimbali za uandishi, ikisaidia wanafunzi kutambua na kuelewa hisia za wahusika. Hii inawasaidia wanafunzi kukuza utambuzi wao wa kihisia na kushiriki kwa kina katika mawasiliano ya kihisia (uk. 22).

Kulingana na data zilizopo kwenye dondoo hili, tunaona kwamba, fasihi inasaidia wanafunzi kukuza huruma kwa kuelewa hisia za wahusika kupitia mbinu mbalimbali za uandishi. Fasihi huwawezesha wanafunzi kuboresha utambuzi wao wa kihisia na kushiriki zaidi katika mawasiliano ya kihisia. Hii inaonesha kwamba

fasihi andishi inakuza uwezo wa utambuzi wa hisia miongoni mwa wanafunzi.

Licha ya haya, kwenye muktadha wa shule teule wilayani Nyanza, fasihi andishi haijatumiwa kwa ufasha kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu, taarifa tulizozipata kutoka kwa walimu kuhusu stadi za mawasiliano hakuna hata mmoja aliyegusia stadi ya utambuzi wa hisia. Hii inatokana na uelewa mdogo wa walimu kuhusu stadi za mawasiliano. Ilibainika kwamba walimu huhusisha stadi ya utambuzi wa hisia katika ufundishaji wake bila kujua. Hutumia mbinu za majadiliano na usimulizi, ambapo wanafunzi hushiriki mawazo na hisia zao kuhusu wahusika wa hadithi walizokuwa wakisoma. Aidha, hutumia mifano ya hali za kihisia kutoka kwa wahusika wa fasihi andishi ili kuamsha hisia za wanafunzi na kuwafanya waelewe hali za kihisia kwa kina. Ingawa walimu hulenga zaidi kwenye maelezo ya kimaudhui, matumizi haya ya mifano yalibainika kusaidia wanafunzi kubaini na kuelewa hisia za wahusika, hivyo kukuza utambuzi wao wa kihisia bila mwalimu kujua. Kwa hiyo, walimu wanapaswa kufanya juhudi za makusudi ili kuendeleza ufahamu wao kuhusu stadi zote za mawasiliano, ikiwamo utambuzi wa hisia. Hii ni kwa sababu kuelewa na kufundisha stadi hizi kwa kina kutasaidia wanafunzi kuboresha mawasiliano yao na kukuza hisia zao kwa usahihi.

**Hitimisho**

Kwa kuhitimisha, licha ya nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, matokeo ya utafiti uliozalisha makala hii yameonesha kwamba walimu wa Kiswahili hawajafanikiwa kutumia fasihi andishi ili kukuza stadi za mawasiliano katika Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wao. Makala imeonesha kwamba walimu wa shule teule hawajumuishi

kikamilifu fasihi andishi katika mbinu zao za ufundishaji; badala yake, wanazingatia zaidi kanuni za fasihi bila kuimarisha mazoezi ya mawasiliano ya kina. Pia, makala imebainisha kuwa tathmini za walimu zinazingatia zaidi stadi za kusoma na kuandika huku zikipuuzia stadi nyingine faafu katika mawasiliano fasaha kama vile stadi ya kusikiliza kwa makini, utambuzi wa hisia na ujasiri. Aidha, makala imedhihirisha kuwa walimu wengi wanakosa kuzingatia mbinu za kukuza ujasiri kama vile kusimulia hadithi fupi na uigizaji wa tamthilia. Vilevile, imejadili jinsi walimu wanavyokabiliwa na ufinyu wa muda uliotengewa somo la fasihi andishi na baadhi yao wanakosa kutumia mbinu zinazowezesha mawasiliano bora.

Kwa hiyo, mambo haya yote yanathibitisha kwamba fasihi andishi haijakuwa na nafasi inayostahili katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani. Hivyo basi, walimu wanahitaji mafunzo zaidi kuhusu mbinu bora za kutumia fasihi andishi katika kukuza stadi za mawasiliano.

## Marejeleo


Atkin, K. (2012). Communicate with Confidence: A Practical Guide. *Dental Nursing*, 8(9), 584-587. Inapatikana katika https://doi.org/10.12968/denn.2012.8.9.584. Ilisomwa tarehe 17 Julai 2024.

Bisamaza, M. (2022). Nafasi ya Hadithi katika Ukuzaji Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza: Mfano wa Shule Teule za Sekondari Wilayani Nyagatare Nchini Rwanda. *CHALUFAKITA*, 4 (4), 5-64.

Erdem, C., Bağcı, H., Koçyiğit, M., Altıner, C., Saykili, A., Polat, M., & Eğmir, E. (2019). *21st Century Skills and Education*. Kocatepe: Cambridge Scholars Publishing.

Ilankumaran, M., & Deepa, P. (2018). Teaching Literature Enhances Communication Skills - A Study with Special Emphasis on Poetry.

In *International Journal of Engineering & Technology*, 7 (3), 210-224.

Johnson, M. (2018). *Literary Analysis and Emotional Intelligence*. Chicago: University of Chicago Press.

Khakasa, L.S. (2018). *Mikakati ya Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi katika Shule za Msingi za Kaunti ya Kakamega Nchini Kenya* (Shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. Inapatikana katika http://ir-library.mmust.ac.ke. Ilisomwa Tarehe 15 Agosti 2024.

Hongoa, A.I. (2018). *Ujengaji wa Mandhari katika Riwaya: Uhusiano wa Matukio na Mtindo* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma

Ngọc, T.T. (2021). Communication Skills and Their Importance in Effective Interpersonal Interactions. *International Journal of Communication Research*, 11(2), 77-85.

Nguyen, H., Warren, W., & Fehring, H. (2014). Factors Affecting English Language Teaching and Learning in Higher Education. *English Language Teaching*, *7*(8), 122-136.

Pearson, J.C., Nelson, P.E. Paul, E., Titsworth, S., & Hosek, A.M. (2017). *Human Communication* (Toleo la 6.). New York, MA: McGraw-Hill Education.

Priyadharshini, J., & Hameed, M.A.M.S. (2018). Developing Communication Skills in English through Literature. *International Journal of Social Science and Humanities Research*, *6*(1), 30-32. Inapatikana katika Http://www.Researchpublish.com Ilisomwa tarehe 17 Julai 2024.

Pradesh, A., Toppo, T., & Philomina, D. (2021). A Study on the Problems in Communication Skills Faced by the Teachers in the Secondary Schools of Namsai District. In *IT in Industry*, *9*(3), 2021.

Rachella, M. (2021). Bridging the Gap: Practical Approaches to Developing Communication Skills in Language Teaching. *International Journal of Language Education*, 15(2), 30-45.

Robbins, S.P., & Judge, T.A. (2007). *Organizational behavior* (12th ed.). Upper Saddle River, Pearson Education.

Scudder, S.F. (1980). *Communication Theory and Practice*. New York: Academic Press.

Seiler, W. J., & Beall, M.L. (2011). *Communication: Making Connections* (7th ed.). Boston: Pearson Education.

Sen, S., Mahendra, A., & Patnaik, P. (2015). *Communication and Language Skills*. Cambridge: Cambridge University Press.

Sharma, M., Devi, M., Dangoria, R., & Jain, V. (2022). Literature Enhances Communication Skills: A comprehensive review. *World Journal of English Language, 12*(3), 157-163 Inapatikana katika https://doi.org/10.5430/wjel.v12n3p157. Ilisomwa tarehe 10 Agosti 2024.

Sridhar, A. (2012). *Developing Communication Skills*. Inapatikana katika https://www.academia.edu/1464158. Ilisomwa tarehe 16 Agosti 2024.

Venkateswar, R.D., & Mohana, C.G. (2015). Enhancing Communication Skills through Language & Literature. *Research Journal of English Language and Literature (RJELAL), 3*(1), 193-198.